SHULE YA UPILI YA GATITU

MTIHANI WA MUHULA WA KWANZA

KIDATO CHA NNE/2015

KISWAHILI 102/2

JINA.....DARASA.....NAMBARI.....

1)UFAHAMU

soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali

Maisha ya binadamu yamepitia katika hatua mbalimbali katika karne kadha zilizopita. Uzalishaji wa kawi, kwa mfano umeshuhudia mageuko makubwa kuanzia enzi za zama kongwe za mawe ambapo mawe yalikuwa nyenzo kuu ya uzalishaji wa kawi na nishati. Mojawapo wa nyanja ambazo zimepiga misamba mikubwa ya maendeleo ni ile ya mawasiliano. Maelezo ya jinsi usafiri wa zamani ulivyotegemea uwezo wa binadamu kutembea kutoka sehemu moja hadi nyingine yanasikika kama kadhia za paukwa pakawa.

Karne tunayoishi ni karne ambayo huenda ikashuhudia maendeleo **yasiyokadirika** katika nyanja hii. Kwa sasa hivi, tarakilishi imekuwa nyenzo kuu ya mabadiliko hayo kutokana na nafasi muhimu inayochukua katika maisha yetu. Tangu azali tumesikia msemo kuwa 'maarifa ni uwezo' . Ukweli wa msemo huu unadhihirika bayana tuangaliapo nafasi ya tarakilishi kama jira ya teknolojia ya habari na mawasiliano au teknohama. Ubashiri wa mtaalamu wa maswala ya habari Marshal Macluhan, aliyebuni dhana ya 'kijiji kitandawazi' katika miaka ya 1960, unaeleka kutimizika. Mwanahabari huyu alieleza imani yake kuwa mawasiliano yanayohusisha mitambo ya umeme yatauunganisha ulimwengu.

Maendeleo makubwa ya wavuti au mdahalishi katika ulimwengu wa sasa yanasahilisha mawasiliano ya jamaa, ndugu na watu wanaoishi maeneo mbalimbali. Kasi ya uenezaji wa maarifa imekuwa ya juu sana. Migahawa ya mdahalishi au vituo vya bwakameme(cybercafés) vimeenea kila mahali. Inahitaji muda mfupi **kusakura** kwenye mdahalishi tovuti ya google, yaani ukifungua anwani ya http//www.google.com, unaweza kupata taarifa zozote unazotamani. Kwa njia hii mtumiaji anapata maarifa muhimu kwa bei nafuu na kwa njia nyepesi na rahisi kuliko kulazimika kubukua mabuku ya kila aina kupata taarifa sawa na hizo.

Ili kuweza kuihifadhi enzi hii ya teknohama pana haja kubwa ya mataifa yetu kuwekeza katika uwanja huu. Serikali zetu zinapaswa kutambua kuwa jamii kutoijua taaluma ya tarakilishi, angaa ile ya kimsingi, ni kama kutojua kusoma katika enzi zilizopita. Kadiri wakati unavyosonga ndivyo ambavyo tarakilishi inavyochukua nafasi muhimu katika maisha yetu.Katika msingi huu basi lazima ziwepo juhudi za kuyaeneza maarifa muhimu kuhusu matumizi yake.Inahalisi kutambua kuwa mtaka cha mvunguni sharti ainame. Ikiwa tunataka nchi yetu iyafaidi matunda ya teknolojia ya leo basi hatuna budi kuwa tayari kuwekeza ipasavyo.

Uwekezaji huo unaenda sambamba na juhudi ya kuhakikisha elimu inayohusiana na masuala ya tarakilishi inasambazwa nchini. Elimu hii ndiyo maarifa ambayo yatakuwa nguzo ya kimsingi ya maendeleo ya nchi siku za usoni. Ni muhimu hata hivyo kutoa tahadhari hapa. Katika jamii nyingi huwepo watu ambao kila panapokuwa **na mvuvumko** fulani hupenda kuitumia hali hiyo kujinufaisha. Huweza kufanya hivi kwa kuanzisha vituo vya kufundisha maarifa dufu ya tarakilishi nia yao ikiwa ni kufaidika kutokana na karo ghali wanazotoza. Licha ya kuwa tunasisitiza umuhimu wa kuwepo na kusambazwa kwa elimu ya tarakilishi,pana haja ya kuwepo na viwango. Lazima serikali ihakikishe kuwa pana viwango vinavyodumishwa. Hii itazuia uwezekano wa kuanzishwa kwa shule ambazo lengo lao la kimsingi sio kuyaendeleza maarifa ya jamii bali kuijaza mifuko ya wachache walioingiwa na shauku ya utajiri.

Ikiwa jamii yetu itataka kutangamana na kwenda sambamba na wakati lazima iwekeze sio kwa mali bali kwa hali kwenye uwanja huu muhimu. Maisha ya kesho yatadhibitiwa kwa kiasi kikubwa na tarakilishi. Leo hii hata biashara inaendelezwa kwa mfumo huu. Huu ndio msingi wa biasharalishi au biashara ya elektroniki (e-commerce) ambayo imeanza kushika kasi ulimwenguni. Biashara ya aina hii inayawezesha makampuni mengi kuwafikia wateja wake popote walipo ulimwenguni. Umbali wa kijiografia sio kikwazo tena kwa kuwa biashara ya aina hii haitegemei makutano ya ana kwa ana kati ya mteja na muuzaji.

Lazima ziwepo juhudi nyingi tu za kusambaza na kuieneza taaluma ya tarakilishi bali pia kuhakikisha kuwa taasisi nyingi zimetarakilishwa ili kwenda sambamba na wakati. Wakati wa kulundika majalada ofisini kama maghala umepita. Hii ni enzi ya teknohama.

Maswali

(a) Ipe taarifa uliyosoma kichwa mwafaka (al. 2)

.....

b)Taja hatua ya kimsingi kabisa ya nishati. (alama 1)

.....

.....

c)Kwa nini kompyuta ni muhimu katika maisha ya leo. (alama 3)

.....

.....

.....

.....

d)Ni kwa jinsi gani utabiri wa Macluhan umeishia kuwa kweli. (alama 2)

.....

.....

(d) Eleza faida zinazotokana na mdahalishi katika maisha ya siku hizi. (alama 3)

.....

.....

.....

.....

.....

e) Eleza maana ya maneno na vifungu hivi kama vilivyotumia katika kifungu ulichosoma. (alama 4)

(i) Yasiyokadirika.....

(ii) Jira .....

(iii) Kusakura.....

(iv) Mvuvumko.....

2)UFUPISHO

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Maelfu ya watu wako hatarini kupoteza maisha yao kwa sababu ya uvutaji sigara. Wataalamu wanasema mtu anayevuta pakiti mbili za sigara kwa siku moja, anapunguza muda wa maisha yake kwa asilimia 30. Inaelezwa kwamba ingawa wavutaji wengi wa sigara katika nchi za Ulaya na Marekani wanapunguza ama kuacha kabisa uraibu huo, wavutaji katika nchi zinazoendelea wanazidi kuongezeka kila kukicha.

Kwa mujibu wa wataalamu, vijana huanza kuvuta sigara kwa sababu ya utundu na kutaka kujua ladha ama mhemko unaosababishwa na sigara. Wengine huanza kuvuta sigara wakifuatisha wacheza sinema maarufu, wanamuziki ama baadhi ya watu wanaowaenzi.

Sigara ama tumbaku husababisha athari mbalimbali kwa watumiaji wake, miongoni mwake yakiwemo magonjwa ya kifua kikuu, kansa ya mapafu ama utumbo na wakati mwingine kifo. Kwa mujibu wa watafiti, watu wanaovuta sigara kwa miaka 20 na zaidi wako hatarini kwa ugonjwa wa kansa ya utumbo. Hii ni kwa sababu moshi wa sigara unaweza kusababisha uvimbe katika utumbo mkubwa na rektamu. Uvutaji sigara unachangia asilimia 80 – 90 ya magonjwa yanayohusiana na kifua ama njia ya hewa ikiwemo kikohozi, pumu, homa ya mapafu na kansa ya mapafu. Mvutaji sigara hushambuliwa mara kwa mara na magonjwa ya koo, mafua na kikohozi kisichosikia dawa.

Uraibu huu pia huchangia asilimia 30 ya vifo vinavyosababishwa na magonjwa ya moyo. Hewa ya 'Carbon Monoxide' iliyopo kwenye sigara inaongeza kiasi cha 'cholesterol'ambayo huziba mishipa ya damu. Uvutaji sigara husababisha kuta za mishipa ya damu zikakamae; hali ambayo ni hatari na inaweza kusababisha mishipa ya damu ipasuke. Kemikali ya 'nicotine' iliyopo ndani ya 'cigar' inaweza kuongeza shinikizo la damu, mapigo ya moyo na kupunguza kiasi cha oksijeni kwenye misuli, hasa ya moyo. Mvutaji sigara anaweza kufa ghafla, kwani mapigo ya moyo yanaweza kusimama ghafla kwa sababu ya shinikizo kwenye moyo wake linalosababishwa na moshi ama kemikali zilizopo kwenye sigara.

Mwanamke anayemeza vidonge vya kuzuia mimba na anavuta sigara anaweza kupatwa na athari kubwa za kiafya na kuhatarisha maisha yake. Hatari zinazomkabili ni pamoja na damu kuganda katika sehemu

za miguuni na katika moyo. Matatizo hayo yanaweza kusababisha athari zaidi wakati wa ujauzito ama wakati wa kujifungua na hivyo kupelekea mama kufa ghafla kabla ama baada ya kujifungua.

Pia, kwa mujibu wa utafiti, watoto wanaozaliwa na akina mama wanaovuta sigara wakiwa wajawazito aghalabu huvuta sigara wakiwa na umri mdogo sana. Tumbaku ama bidhaa zinazotokana na tumbaku huweza kupenya katika plasenta kwa kuingia katika mfumo wa damu ya mtoto aliye tumboni na hatimaye katika ubongo na hivyo kupelekea mtoto huyo ajaribu kuvuta sigara akiwa na umri mdogo. Uvutaji wa sigara kwa mama mjamzito unaeleweka wazi kwamba humuathiri mtoto aliye tumboni kwani huathiri ulimi na kuwafanya wawe na uzito kuongea na pia huwa wazito kujifunza na huathiri mapafu yao katika siku za baadaye za uhai wao.

Nchini Kenya, Serikali sasa inapanga kuanzisha mbinu na sheria za kuhakikisha kuwa wavutaji sigara hawavuti katika maeneo ya umma. Sheria hizo zinapiga marufuku uvutaji sigara kwenye maeneo yote ya umma. Tayari, taasisi mbalimbali za umma na za kibinafsi zimeandika mabango ya kuwaonya wavutaji dhidi ya kuvuta sigara katika mazingira ya taasisi hizo.

Maswali

(a) Bila kubadilisha maana, fupisha aya nne za kwanza. (Maneno 60 - 65) (al. 7.Mtiririko 1)

Matayarisho

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

Nakala safi

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

(b) Kwa maneno 55-60 fafanua athari za uvutaji sigara kwa wanawake. (al. 6 mtiririko 1)

Matayarisho

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

Nakala safi

.....

.....

.....

.....

.....

.....

3)MATUMIZI YA LUGHA

a)Sahihisha. (al. 2)

Wageni wenye walikuja walikula wali na vijiko

.....

.....

b)Ipe vokali i sifa zake tatu (al. 3)

.....

.....

.....

c)Weka nomino hizi katika ngeli zake. (al. 2)

(i)mali.....

(ii)utukutu.....

d)Tumia kirejeshi amba kuunganisha mafungu yafuatayo (al. 2)

Mwanafunzi Yule ni mwerevu. Mwanafunzi yule amejiunga na chuo kikuu.

.....

.....

e)Eleza aina za virai vilivyopigiwa mstari. (al. 2)

Miti ilipandwa <u>kando ya mto</u>

.....

Tajiri <u>mwenye gari kubwa</u> amewasili.

.....

f)Andika upya sentensi hii ukifuata maagizo mabanoni (al. 2)

Kazi hii imekuwa ngumu kwangu. (Malizia kwa..... ngumu)

.....

g)Geuza katika ukubwa wingi (al. 2)

Kijito hiki kinatiririka kutoka katika kilima kile.

.....

.....

h)Ainisha mofimu katika neon **yaliyosahaulika** (al.3)

.....

.....

.....

i)Unda nomino mbili kutokana na kitenzi kera (al. 2)

.....

.....

j)Onyesha aina za shamirisho katika sentensi hizi. (al. 3)

Nyumba ya matofali inayojengewa wazee itakamilika mwezi ujao.

.....

.....

.....

k)Ainisha vitenzi. (al.2)

Hajawahi kunipatia pesa zozote.

.....

.....

l)Andika katika usemi halisi. (al. 2)

Mutua alimshukuru Ann kwa kumletea zawadi.

.....

.....

m)Tunga sentensi ukitumia **fauka ya** (al. 1)

.....

.....

n)Eleza matumizi ya **ku** katika sentensi: (al. 2)

Hukufikisha ujumbe kama alivyokutuma.

.....

.....

o)Changanua sentensi hii kwa njia ya matawi. (al. 4)

Ruto alikimbia hadi akampata Asha.

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

p)Tunga sentensi kudhihirisha maana ya maneno yafuatayo. (al. 2)

(i)fumba

.....

(ii)vumba

.....

q)Andika katika kinyume. (al. 2)

Kamene anapenda kutii maagizo

.....

r)Tunga sentensi ukutumia neon **chafu** kama (al. 2)

(i) nomino

.....

(ii)kivumishi

.....

4)ISIMU-JAMII

Eleza sababu tano zilizochangia kuenea kwa Kiswahili nchini baada ya uhuru. (al 10)

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....